JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

*Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa:*

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**S.L.P. 70,**
**SIKONGE,**
**TABORA.**

**Tel:** +255 659 566703 (Direct line)
***e-mail:*** **ded@sikongedc.go.tz**
**TOVUTI: www.sikongedc.go.tz**

**28/02/2022**

***TANGAZO LA KUOMBA NAFASI ZA UJUMBE WA UWAKILISHI KWA VIJIJI WANACHAMA WA JUMUIYA YA HIFADHI YA WANYAMA PORI IPOLE.***

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inawatangazia wananchi wote kutoka kwenye vijiji wanachama wa Ipole, Ugunda, Utimule, Msuva,Idekamiso na Mwamulu kuomba nafasi za ujumbe uwakilishi kwenye Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyama pori Ipole.

**SIFA ZA MWOMBAJI.**

I. Awe na elimu ya darasa la saba na kuendelea (wenye kidato cha nne watapewa kipaumbele)
II. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 au zaidi na wenye akili timamu.
III. Awe na uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu na awe na upeo wa kutafsiri na kuelewa mambo.
IV. Awe hajewahi kuhukumiwa kwa makosa ya jinai.
V. Asiwe na wadhifa wowote katika Serikali ya Kijiji, vyombo vya dola, mtumishi wa Serikali au uongozi wa vyama vya siasa.
VI. Awe ni mwanakijiji mkazi wa kijiji mwanachama kwa muda usiopungua miaka mitano.
VII. Awe Raia wa Tanzania.

**MAOMBI YAAMBATANISHWE NA VIELELEZO VIFUATAVYO:**

I. Nakala ya cheti cha darasa la Saba.
II. Nakala ya cheti cha kidato cha nne.
III. Picha mbili za passport size.
IV. Nakala ya Kitambulisho cha Nida/ kitambulisho cha mpiga kura.
V. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono, zikiwa na anwani kamili ya Mwombaji, namba za simu, barua pepe na ziwasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Kwa anwani

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE,
S.L.P 70,
**SIKONGE.**
Au kwa barua pepe ded@sikongedc.go.tz
**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 6/3/2022 saa 5:59 usiku.**

Yusuph Hamza
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA SIKONGE

Scanned with CamScanner